

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA

07 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA TISA – TAREHE 07 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

343. MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kupandisha hadhi Zahanati ya Kijiji cha Sojo kuwa Kituo cha Afya.

344. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi katika makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**345. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT
KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Wananchi wa Jimbo la Nkenge, ambao hawajapata Vitambulisho vya Taifa au Namba za Usajili watapatiwa vitambulisho.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**346. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS
KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, Serikali ina kauli gani kwa Wananchi wa Kipunguni waliozuiwa kuendeleza maeneo yao kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege.

WIZARA YA MAJI:

**347. MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA
(MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mradi wa maji Kata ya Iwawa Makete Mjini.

**348. MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE
(KILWA KASKAZINI):**

• Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:- •

Je, ni lini mradi mkubwa wa maji kutoka Mto Rufiji utaanza kutekelezwa.

**349. MHESHIMIWA BUPE NELSON
MWAKANG'ATA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Mradi wa maji wa Ikozi uliopo Sumbawanga Vijijini utakamilika.

WIZARA YA KILIMO:

**350. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini Vyama vya Maendeleo ya Ushirika vya Zao la Mchikichi vitaanza kufanya kazi katika Mkoa wa Kigoma.

WIZARA YA NISHATI:

**351. MHESHIMIWA ESTHER LUKAGO MIDIMU
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha kuweka umeme katika Vijiji 138 vilivyobaki vya Mkoa wa Simiyu.

**352. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO
(BABATI VIJIJINI):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Qameyu, Madunga na Kiru Babati Vijijini.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.



DODOMA
07 JUNI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE